

Aprili 12, 2020

Wapendwa Familia za JCPS:

Tunatumai umefurahia wikendi na u tayari kwa wiki nyngine kuu ya Mafunzo Yasiyo ya Kiasili (NTI). Asante kwa msaada wako na kujitolea kwa mtoto wako wakati huu muhimu. Haya ni baadhi ya mambo ya kukumbuka tunapojitayarisha kwa wiki yetu ya pili ya NTI.

Msaada wa Nywila ya Mwanafunzi

- Ikiwa unahitaji msaada na nywila yako ya mwanafunzi ili kuingia kwenye Google Classroom au ikiwa una maswali kuhusu kuingia, tafadhali wasiliana na shule ya mtoto wako.
- Unapowasiliana na shule ya mtoto wako, utahitajika kuwacha ujumbe na mtu kutoka shule atakupigia simu. Tafadhali toa ujumbe ufuata ounapowacha ujumbe.

Jina langu ni _____ (*jina lako*).

Jina la mwanafunzi wangu ni _____ (*jina la mwanafunzi*).

Mwanafunzi wangu ako katika daraja _____.

Ninahitaji msaada na _____ (*nywila ya mwanafunzi wangu, kuingia kwenye Goggle Classroom*)

Nambari yangu ya simu ni _____ (*nambari bora zaidi ya kunifikia*).

Wakati bora zaidi wa kunipigia ni _____ (*wakati mtu anaweza nipata kwa urahisi*).

Anwani ya Mwalimu

- Ikiwa mtoto wako bado hajawasiliana na mwalimu/walimu, tafadhali wasiliana na mwalimu kupitia barua pepe au wacha ujumbe katika shule na ujuishe habari iliyoorodheshwa hapo juu.

Shiriki Hadithi Zako Nasi!

- Tunapenda kuona wanafunzi wako wakishiriki kwa kusoma, san asana katika NTI. Shiriki kufanikiwa kwa familia yako katika NTI kwenye vyomb vya habari kwa kutumia #WeAreJCPSAtHome. Usisahau kufuata JCPS katika Facebook(Jefferson County Public Schools), Twitter (@JCPSKY) na katika Instagram (@JCPSKY) kwa habari mpya za wilaya.

Unapoamua ratiba bora ya familia yako katika NTI, tafadhali fahamu kuwa walimu wetu na wakuu watakuwa wepesi kutimiza mahitaji yako. Mnafanya kazi njema zaidi familia za JCPS!

Kwa dhati,
Mawasiliano ya JCPS